# <u>JITIHADA ZAFUA DAFU</u> - Wanyenya Willy

## <u>MTIRIRIKO</u>

### Sura ya 1

Masombo na familia yake wako katika pilka pilka za kuandaa karamu pale nyumbani baada ya sherehe za kufuzu. Miaka miwili iliyopita Masombo alikuwa katika chuo kikuu cha Hussein Musa pale mjini Mbale akisomea kozi ya uzamili katika Kiswahili. Masombo alishirikiana na jamaa na marafiki kufanya maandalizi pale kwao.

Kabla ya siku hiyo ya sherehe , masombo aliota kwamba yuwachekwa sana na majirani kwa sababu ya umaskini waliokuwa nao. Katika ndoto hiyo aliondoka hadi mjini, kupitia jangwani kwenye wanyama hatari. Pale mjini alipata mhisani mmoja aliyemtafutia kazi akatajirika na kununua Benzi na Lori kubwa la mizigo. Alijenga nyumba kubwa na hata kusafirisha familia yake hadi mjini. Majirani waliomcheka walishangaa. Alipozindukana ndotoni, akagundua kuwa ilikuwa tu ndoto.

Shughuli zilipomalizika Masombo alikuwa amekodisha magari matatu, Benzi moja lake na familia yake na mawili ya jamaa na marafiki. Akakumbuka alivyopitia maisha magumu na alivyolazimishwa kuoa akiwa kidato cha tatu. Alifukuzwa shuleni na kuanza maisha kama mme utotoni. Nyumba, chakula , mavazi vikawa ni ndoto kwake. Kwa bahati nzuri Mwalimu Mkuu wa shule ya upili ya Bukigai akamwajiri kama mwalimu msaidizi. Masombo alijiwekea pesa na kuamua kurudi shuleni kuendelea na masomo. Alifanya mtihani wa kidato cha nne akapita na kujiunga na kidato cha tano na baadaye kufanya mtihani wa kidato cha sita.

Ingawa hakupita vizuri sana katika kidato cha sita, alijiunga na chuo cha kufunzia walimu wa shule za upili cha Musese na kufuzu baada ya miaka miwili. Baada ya kufanya kazi na kujiwekea pesa akijiunga na Chuo Kikuu cha Makerere na kufanya Kiswahili katika taaluma ya Elimu. Hakukomea hapo, baada ya kufanya kazi kwa bidii akajiunga na chuo kikuu cha Hussein Musa na kufanya kozi ya uzamili katika Kiswahili. Kufuzu katika kozi hii kulimfurahisha sana ndipo maskini wa Mungu akaandaa sherehe kubwa.

Siku ya sherehe ilipofika, rafiki yake wa dhati Omari, mzanzibari alijitolea kumpa Benzi la kumbeba yeye na familia yake. Omari na Masombo walisaidiana sana wakiwa chuoni. Kabla kuondoka Masombo aliomba, na msafara wa magari ukafuatana hadi chuoni kwa sherehe za kufuzu. Majirani wakashangaa wengi wao wakiwa na chuki pamoja na huzuni.

Walipofika chuoni, walichukua viti vyao katika mahema. Mgeni wa heshima Profesa Bakari

Uthimani na viongozi wengine wakaingia na kuendesha sherehe za kufuzu kwa shangwe na vigelegele. Sherehe zilipoisha Masombo na wageni wake wakarudi nyumbani na kuanza karamu yao. Hotuba mbalimbali za pongezi zilitolewa, watu wakala vyakula vya kila aina na vinywaji kwa shangwe na vigelegele. Wakaburudika hadi mwendo wa saa sita usiku.

## Sura ya 2

Masombo alizaliwa pamoja na ndugu zake sita. Hata hivyo ndoa ya wazazi wake ilivunjika wakiwa watoto na mamake akatokomea. Babake Masombo (Mzee Kibeti) alikuwa mlevi wa gongo, hivyo Masombo na ndugu zake wakateseka sana kwa kujifanyia kila kazi pale nyumbani. Ndugu yake mmoja aliaga dunia kwa homa ya malaria baada ya baba yao kukosa kumpeleka hospitalini. Hata hivyo, kwa sababu kulikuwa na uchawi sehemu hiyo, babake akaamini kwamba mtoto huyo alirogwa.

Watoto hawa walipoteseka sana, Mzee Kibeti akaamua kuoa mke wa pili ili labda awalee. Kinyume na alivyotarajia, mama wa kambo aliwafanyia vituko. Aliwapa kazi ngumu, kuwapiga pamoja na kuwanyima chakula. Mzee Kibeti alimuogopa mke wake wa pili sana. Hakuwatetea watoto wake. Tunao Mzee Kibeti akimfichia Masombo chakula ili ale kisirisiri. Mama wa kambo alipogundua, akazua rabsha wakapigana vibaya sana pale nyumbani.

Masombo na ndugu zake walilala njaa siku kadhaa kwa sababu hata ombaomba zao kwa majirani hazikufua dafu. Tabia hizi za mama wa kambo zilipozidi, Mzee Kibeti akaamua kumrudisha mkewe wa kwanza. Masombo alipelekwa shule ya msingi ya Bukigai alipotimia miaka saba. Kwa sababu ya bidii zake shuleni, Masombo akaonyesha umaarufu katika kusoma, kuandika na kuhesabu. Akapendwa na Mwalimu wa hisabati sana kiasi cha wanafunzi wenzake kumchukia darasani. Siku moja Kutosi, mwanafunzi mwenzake alipanga njama na wanafunzi wengine na kumuaibisha Masombo darasani kwa kumsingizia kuwa alichafua hewa.

Ukweli ulipodhihirika, Kutosi na wenzake walichapwa viboko ishirini kila mmoja na kupewa kazi ngumu. Kuanzia siku hiyo, Masombo aliwachukia wenzake sana kwa kumwonea wivu. Lakini mwalimu wake huyo wa Hisabati alimshauri na kumhimiza kuwasamehe wenzake. Wanafunzi hao wakabadilika na kusaidiana kimasomo hadi wote wakapita katika divisheni ya kwanza. Mwaka uliofuata Masombo akajiunga na shule ya upili ya Masaaba kule Bugisu.

## Sura ya 3

Bidii na ufanisi wa Masombo kimasomo ulileta chuki baina ya Masombo na majirani zake. Wengi wao walimwonea kijana huyu wivu na hata waliomwonyesha furaha walijifanya tu. Baadhi ya jamaa zake wa karibu na watu wa ukoo wake waliostahili kumsaidia waliungana na maadui na kumtakia mabaya. Tunaona siku moja Ami zake wawili wakimwambia wazi kwamba wao hawataki kushirikiana na wasomi kufanya kazi pale kijijini.Wakati huo babake Masombo alikuwa

ashafariki dunia. Masombo alijawa na huzuni sana. Mamake Masombo alikuwa anafahamu tabia hizo za shemeji zake. Inasemekana hata Mzee Kibeti alipokuwa hai walimchukia eti kwa sababu alimiliki ngombe watano, ekari moja ya shamba na kusoma hadi darasa la tano.

Mamake Masombo alimuhimiza kusoma kwa bidii na kuepukana na jamaa zake. Usiku huo Masombo akaota akiwa jangwani katikati ya majabari mawili mawili makubwa yaliyokuwa magumu kuyapanda. Lakini kule mbali aliyaona mazingira mazuri nay a kupendeza.

Mamake Masombo alikuwa maskini wa kupindukia. Kifo cha mmewe pia kilikuwa pigo kubwa, akawa ndiye kichwa cha familia. Alianza kazi ya kupika na kuuza pombe haramu ya changaa ili kutafuta chakula na karo ya watoto wake. Shule zilipofunguliwa, Masombo akajitayarisha kuingia kidato cha kwanza katika shule ya upili ya Masaaba. Aliandamana na mamake wakatembea karibu kilomita mbili kwenda shuleni huku wamebeba sanduku zito na godoro. Masombo aliripoti shuleni miguu mikavu bila viatu, wenzake wakamcheka sana. Hata binamu yake aliyekuwa na jozi kadhaa za viatu alikataa kumuazima. Mamake alirejea nyumbani bila hata kumwachia shilingi moja. Tayari wanafunzi walikuwa wamepata chajio, hivyo, Masombo akalala njaa.

Masombo alivumilia maisha magumu pale shuleni. Hata hivyo baada ya majuma matatu, shule hiyo ikafungwa kwa ghafla, kwa kuhofia kuzuka kipindupindu. Inasemekana baadhi ya walimu hawakumpenda Mwalimu Mkuu, hivyo wakachochea wanafunzi wakajaza vyoo kwa takataka. Masombo hakuwa hata na nauli ya kumrudisha nyumbani, hivyo akakanyaga miguu kwa masaa saba hadi kwao.

Muhula wa pili ulipoanza, Mwalimu Mkuu alifanya mabadiliko mengi ili kuboresha maisha ya wanafuzi. Chakula kilikuwa kizuri, burudani na vile vile michezo mbali mbali kuanzishwa. Hata hivyo watoto wa matajiri hawakuridhika.

Maisha magumu yalimfanya Masombo kufanya bidii masomoni, kwa sababu alitambua kwamba elimu ndiyo ufunguo wa maisha. Hata hivyo, Masombo alipofika kidato cha tatu alibadilika kabisa labda kutokana na umri . Akaachana na vitabu na kuanza kumangamanga na wasichana kwa shughuli ya mapenzi.

## Sura ya 4

Siku moja wakati wa likizo Masombo alimdanganya mamake kwamba ameenda kuwatembelea wajomba zake, kumbe kaenda kumwona kipenzi chake Sijali. Msichana huyu alikuwa mrembo kupindukia tena mtu wa ukoo wao. Masombo kufika huko, akamtuma Sema akamwitie Sijali.

Sijali alifika kwa haraka na kujifungia chumbani na Masombo kwa ajili ya kufanya mapenzi. Lakini ghafla bin vuu bibie Sijali alikuwa tayari ashagundua njama zao. Alifika pale nje na kubisha haraka. Masombo kuona vile, akafungua haraka na kuponyoka. Alitoroka moja kwa moja hadi kwa wajomba na kujificha kule hadi usiku.

Aliporudi kwao usiku akapata habari kwamba kijiji kizima kilikuwa kimegundua visanga vyake. Kwa kuogopa aibu, Masombo akapanga mizigo yake na siku iliyofuata asubuhi, akaondoka hadi shuleni kwani likizo lilikuwa limeisha.

Hata hivyo, tabia hiyo ya Masombo hakuibadilisha. Wakati wa likizo aliendelea kufanya mapenzi kiholela na wasichana kadhaa kijijini pamoja na wanawake. Mzee Mayeku na wengine pale kijijini walimlalamikia mamake sana kuhusu tabia ya Masombo. Mamake akamshauri na kumuonya hadi Masombo akaomba msamaha. Hata hivyo Masombo alitaka tu kumfurahisha mamake, hakubadilika kamwe. Walipokuwa shuleni, alikuwa na kipenzi chake nabuduwa. Nabuduwa alikuwa kiongozi wa wanafunzi katika shule jirani ya Budadiri. Masombo na Nabuduwa walikuwa wakihepa usiku usiku wakienda mjini Mbale kuburudika. Kwa sababu Nabuduwa alikuwa mtoto wa tajiri, alifadhili kila kitu.

Kwa bahati mbaya Nabuduwa akapata mimba wakiwa katika kidato cha tatu na kufukuzwa shuleni. Masombo akatafutwa shuleni na Polisi na kukamatwa. Walipotaka kumtia pingu, akazua vita na kumpiga Polisi. Hata hivyo, walimshinda nguvu na kumtia mbaroni kwa mashtaka mawili;

(a) Kumtunga mimba msichana mdogo – kifungo cha miaka 15.

(b) Kushambulia polisi – kifungo cha miaka 5

Ili kufililisha hiyo kesi, Afisa wa polisi aliitisha kitu kidogo. Mamake Masombo na ndugu yake Mwema walilia sana. Ikabidi mamake auze kila kitu; ngombe, mbuzi, kuku, nguo zaken.k Akamtuma Mwema kulipa laki saba pamoja na kuwahonga wazazi wa Nabuduwa pale kwenye kituo cha polisi. Masombo akalazimishwa kuoa akiwa kidato cha tatu. Masomo yakaisha. Mamake alijifungia chumbani akilia kwa kuuza kila kitu na kubakia uchi. Masombo na Nabuduwa wakaanza uchumba utotoni. Nyumba, chakula, mavazi, vyombo vya matumizi…vikawa ngumu kupata. Majirani wakamtia fitina Nabuduwa awachane na Masombo lakini akakataa. Walikula majani ya mwitu kama mboga na wakati mwingine kulala njaa. Asiyefunza na mamake kweli hufunza na ulimwengu.

## Sura ya 5

Masombo alifanya vibarua kijijini usiku na mchana ili kupata mkate wa kila siku. Usiku mmoja Nabuduwa akashikwa na maumivu ya uzazi. Hospitali ilikuwa mbali sana. Usiku huo Mwema na Masombo wakaamua kumbeba Nabuduwa na kutembea naye hadi hospitalini. Tunamwona mama yao akitoa maombi kwa mababu zao hasa Masaaba awaongoze kwa Baraka. Barabarani walikumbana na majambazi karibu wauliwe.

Kule hospitalini askari wa lango anahongwa shilingi elfu kumi ili awaongoze hadi kwenye wadi. Kwa bahati nzuri, Nabuduwa akazalishwa na wahisani fulani pale. Masombo akatoa shati lake na kukifungia kitoto kwa kukosa taulo.Mkunga alipoingia, anaitisha hongo kabla kuwasaidia na wanapokataa anawatusi na kuwafukuza. Wakabeba kitoto hicho hadi nyumbani.

Mzee Shibita alialikwa pale nyumbani ili kufanya sherehe ya kukipa kitoto hicho jina kimila. Akajenga chumba kidogo cha kafara pale nje pamoja na kumchinja mbuzi beberu ambaye alichomwa na kutolewa mababu zao. Baada ya sherehe hiyo, kitoto hicho kikapewa jina Nabwire.

Malezi ya mtoto huyo yalikuwa magumu sana. Hakukuwa na mavazi, maziwa, na pesa za matibabu. Mtoto alipougua Masombo aliingia mwituni na kutafuta Mitishamba kama dawa. Majirani waliokuwa na kila kitu waliwacheka tu. Nabuduwa na Masombo wakafanya vibarua kwa pamoja ili kulea mtoto wao. Waliwalimia majirani zao usiku na mchana ili kupata hela.

## Sura ya 6

Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi ya Bukigai, Bwana Joshua Kimanayi alikuwa mtu mzuri sana. Asingetaka kuona mtu akiteseka. Tunamwona akitumanisha Masombo aitwe ili aone jinsi ya kumsaidia. Kimanayi alimwajiri Masombo Kama mwalimu msaidizi katika shule yake. Masombo akapewa mshahara wa kwanza ili ajiandae kufanya kazi.

Alipitia sokoni akajinunulia nguo, pamoja na kumnunulia mkewe , mtoto wao na mamake mzazi. Masombo akangara na kununua vitu vya nyambani. Majirani wakaanza kufanya urafiki naye na hata kumtembelea  ili awasaidie. Wasichana pia wakaanza kumtamani tena. Hata hivyo, Masombo alimpenda mkewe pekee.

Masombo alipata mshahara akajenga nyumba ya mabati. Majirani wakamchukia na kumwonea wivu. Kamati moja iliundwa pale kijijini kusimamia kusimamia mradi wa serikali wa kufuga ngombe. Masombo akapewa nafasi ya ukarani, watu wakapinga na kuondoa jina lake uongozini. Walidhani kuwa nafasi hiyo itamtajirisha Zaidi. Masombo kuona hivyo, akatahadhari na majirani.

Mamake Masombo (Namutosi) aliamua kusafiri hadi Mombasa Kenya kutafuta kazi. Masombo akampa nauli ya shilingi elfu hamsini. Baada ya miezi sita, Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi ya Bukigai akabadilishwa kukaja Mwalimu Mkuu mgeni aitwaye Mjanja. Mjanja alikuwa mjanja kweli kama jina lake. Tunaona Mjanja akipanga njama na kuwaibia walimu mshahara waliokuwa wakidai serikali kwa miezi kumi. Masombo aliyemsaidia katika njama hizo za wizi hakupata chochote. Ikizidi mshahara wa Masombo pia ukaibiwa Mjanja akidai kuwa jina la Masombo limeondolewa katika daftari la wafanyi kazi.

Masombo kuona hivyo, akazua vita na kumpiga huyo Mwalimu Mkuu ofisini mwake. Masombo aidha alimwandikia afisa mkuu wa Elimu wilayani na kumfahamisha kuhusu kashfa hiyo ya Ghost teachers katika shule hiyo ya Mjanja. Mjanja kuona hivyo, akamwita Masombo na kumpa mshahara wake. Hata hivyo, alipoteza kazi yake.

Masombo akaona badala ya kukaa nyumbani ni heri arudi shuleni aendelee na masomo. Akajiunga na shule ya upili ya Nalwanza katika kidato cha tatu, akiwa na miaka 30. Alisoma kwa bidii na kuibuka kuwa mwanafunzi bora, akafadhiliwa na shule kwa kugharamia karo yote. Kwa sababu ya kusoma sana, majirani walimbandika jina Bwana mabuku. Masombo alipita mtihani wa kidato cha nne vizuri sana na kujiunga na shule ya upili ya Bukalasi alikofanyia kidato cha sita.

Ingawa hakupita vizuri sana, aliingia Chuo cha Kitaifa cha walimu cha Musese na kufuzu na sitashahada ya Ualimu. Akaajiriwa katika shule ya upili ya Bududa, na baada ya kujiwekea pesa kwa miaka sita, akajiunga na Chuo Kikuu cha Makerere, kuendelea na Masomo. Baada ya kupata shahada, akaajiriwa kama mwalimu katika shule ya upili ya Bushiko.

Baada ya muda mfupi, juhudi zake zilimfanya kupandishwa cheo na kuhamishiwa shule ya upili ya Bukigai karibu kwao. Wakati huo Bw. Mjanja alikuwa amestaafu na alifanya kibarua kama msimamizi wa wafyeka nyasi pale shuleni. Alikuwa amekonda na kuonekana mchafu sana. Bw. Mjanja alipogundua kwamba Masombo sasa ni bosi wake, akaomba msamaha. Masombo kwa wema wake akamsamehe na kumpa kazi ya kufundisha pale. Masombo akampa laki tano za bure ili zimwezeshe kujiandaa kuanza kufundisha Kiingereza.Masombo alipotambua umuhimu wa elimu, akaamua kumrudisha mkewe Nabuduwa shuleni. Wakati huo, mkewe alikuwa mama wa watoto sita.

## Sura ya 7

Masombo aliamua kuingilia sana dini, na kueneza neno la Mungu. Mzee Kibeti na mkewe Namutosi, inasemekana kuanzia zamani, walikuwa waumini katika kanisa la kiangilikana la Bukigai. Hata hivyo, kulikuwa na chuki baina ya viongozi wa kanisa haswa makasisi. Tunamwona kasisi Mukhwana aliyekuwa akijulikana sana na kuwavutia waumini katika mahubiri yake, akifanyiwa fitina na Makasisi wenzake. Baadaye akahamishwa, jambo

lililowahuzunisha sana wafuasi na wakristo kwa jumla.

Masombo aliongoza ibada kwa jumapili kadhaa, na kasisi mwingine Mzee Kibogoyo alipoletwa pale, wakristo wa Bukigai wakamkataa. Vile vile, makasisi hao walianza kumpiga vita Masombo. Kwa kudai kwamba anawapotosha wakristo wa Bukigai na kuwachochea. Masombo kuona hivyo akalihama kanisa hilo na kujiunga na kanisa la Wakristadelphiano ambalo lilifadhiliwa na wazungu kutoka Uingereza.

Hata hivyo, viongozi wa kanisa hili walikuwa wafisadi mno. Pesa zilizotumwa kwa ajili ya kuwasaidia wakristo, zilifichwa na viongozi hawa huku wakituma ripoti bandia kwa wazungu. Uchaguzi wa wanakamati wapya ulipofanyika, Masombo akapewa nafasi ya Afisa wa Misaada nchini.

Kinyume na watangulizi wake, Masombo akatumie zile pesa za misaada kwa uwazi na utaratibu. Ripoti zake zilipendeza sana wazungu na wafadhili kwa jumla. Wazungu wakamtumia Masombo hela za kujengea kanisa jipya katika eneo lake kwa sababu ya uaminifu wake. Wakristo kuona hivyo, wakaona wivu na kukataa hata kumuuzia Masombo shamba la kujenga kanisa hilo. Wakaanza kusambaza propaganda na uvumi kuwa kanisa hilo linaabudu mashetani. Kwa bahati nzuri, Masombo akauziwa kijishamba na kijana mmoja ambaye alikuwa anahama eneo hilo kwa kufiwa na watoto wake mfululizo. Inasemekana kijana huyo alikuwa akiishi na wajomba zake pamoja na mkewe, jambo ambalo ni mwiko. Pesa za kujenga kanisa zilitumwa na ujenzi kuanza kwa haraka sana. Wakristo wa makanisa mengine kuona hivyo wakaona wivu sana.

## Sura ya 8

Baada ya muda fulani wakristo wa kanisa hilo wakabadilika na kuanza kumchimba Masombo ili wamuondoe cheoni. Baadaye, Masombo alipojenga nyumba kwa pesa zake, wakadhani anawaibia. Masombo kuona hivyo, akajiondoa na vijana fulani wakachaguliwa kusimamia pesa za misaada.

Kusolo alichaguliwa kama mwenyekiti. Baada ya muda mfupi Kusolo alishirikiana na wanakamati wengine na kuwaibia wakristo pesa za misaada. Wanakamati hawa waliiba hata pesa za kuwakaribisha wazungu wanaowafadhili. Wakakopa madeni mengi kwa ajili ya kukaribisha wageni, karibu kanisa hilo kufungwa kwa madeni. Wakristo walipogundua dhuluma hizo wakakataa kamati hiyo na kumwomba Masombo arudi tena ushukani.

Masombo alijaribu kumshauri Kusolo kuhusu kilio cha wakristo lakini Kusolo akadhani kwamba

Masombo ndiye anayewachochea wafuasi. Tunaona Kusolo akimgombanisha na hata kumtusi. Masombo akavumilia na Kushirikiana nao kama katibu. Walipotaka kumwondoa kwenye kamati wakashindwa kwa sababu Masombo ndiye aliyeweka kumbukumbu za kamati. Akawasaidia kufungua akaunti.

## Sura ya 9

Aliposumbuliwa sana Masombo akaamua kuanzisha tawi jipya la kanisa hilo mjini Mbale ili kuepukana na wakristo wa Bukigai. Uamuzi huu aliufanya baada ya kushauriana na mzungu Mathias, aliyekuwa mfadhili. Mathias alipowatembelea kutoka ngambo, akaufadhili mradi huo kwa furaha na kuwafahamisha wakristo. Hata hivyo Nabende akishirikiana na wakristo wengine wakamfanyia fitina Masombo kwa Mzungu. Wakadai kwamba Masombo ni mbinafsi na hawezi kuongoza kanisa la Mbale. Aidha walidai kuwa Masombo humpiga mkewe kila siku, jambo ambalo lilimkasirisha sana mzungu.

Masombo na dadake Sarah walikuwa wamekodi nyumba kule Half London mjini Mbale ili kuanzisha tawi hilo la kanisa. Lakini kwa sababu huko kulionekana kwa matajiri akawashauri wahame. Wakatafuta nyumba mbili ndogo katika mtaa wa Namatala kunakoishi maskini. Kanisa liliimarika baada ya miezi miwili na Masombo kupata wafuasi wengi sana.

Wazungu walipoanzisha shule ya chekechea kule Bukigai, wakamteua Masombo kama katibu katika kamati tendaji. Shule hiyo ikapewa ufadhili kutoka Canada. Hata hivyo, Masombo na wanakamati wengine wakaanza kula pesa. Masombo alishirikiana na Makosia na Nabende wakaiba pesa na kuandikia wazungu ripoti na risiti bandia.

Masombo hata hivyo akaamua kuepukana na dhambi hizo kwa kujiuzulu. Akaamua hata kumwandikia mzungu barua kumfahamisha jinsi wanakamati huiba pesa. Mzungu aliwatembelea mara moja na kutaka kujua namna pesa hizo hutumiwa. Akaitisha mkutanao na kamati tendaji ili wamuelezee matumizi ya pesa. Wanakamati wengine walikataa kwamba hawaibi pesa, kumbe mzungu alikuwa na habari kamili. Masombo akatoboa siri yote wakaaibika. Nabende na Makosia wakakasirika sana. Mzungu aliporudi Canada akasimamisha misaada.

## Sura ya 10

Masombo akajiunga na Chuo Kikuu cha Hussein Musa na kusomea kozi ya uzamili katika Kiswahili. Ingawa watu walimcheka na kudhani kwamba asingemaliza kozi yake, Masombo alisoma kwa bidii na baada ya miaka miwili akafuzu. Baada ya kufuzu, akawa na maadui Zaidi, hasa walimu wenzake.

Masombo akaajiriwa na chuo Kikuu cha Makerere kama mhadhiri. Majirani wakaudhika sana na hata kuanza kumfanyia urogi. Masombo alipewa jumba kubwa chuoni lililokuwa na kila kitu. Akasafirisha familia yake hadi Kampala kwa Lori. Maisha yao yakabadilika. Mkewe Namuduwa alikuwa sasa ni mwalimu wa msingi kule Nakapiripirit. Jirani yake Karimu na mkewe Fatuma waliwakaribisha kwa furaha na kuwaandalia chakula kizuri. Karimu akaahidi kumsaidia Masombo kumhamisha mkewe kutoka Nakapiripirit hadi Naguru jijini Kampala. Tunawaona kwa ukarimu wakiwapa gari lao moja ili watumie.

Shule zilipofunguliwa, Nabuduwa akaanza kufunza Naguru Primary School. Masombo na mkewe waliishi maisha ya hali ya juu kama wazungu. Baada ya kupata pesa zao wakanunua gari lao kubwa na kurejesha lile la Karimu. Masombo akajiunga tena na Wakristadeliphiano na kuanza kueneza injili.

## Sura ya 11

Masombo na mkewe Nabuduwa waliomba ruhusa ya kwenda Mombasa kumwona mamake. Walipofika huko, walishangaa kuona mamake amepiga hatua kimaendeleo. Kutokana na bidii yake, sasa alikuwa na jumba kubwa lililokuwa na kila kitu. Mamake akawakaribisha na kuwapongeza kwa juhudi zao. Akawatembeza mjini Mombasa kwa gari lake aina ya Premio.

Masombo na mkewe walimtaka mama yao kuandamana nao hadi Kampala, lakini haikuwezekana kwa sababu alidai kuwa ana shughuli nyingi. Masombo na mkewe wakarudi Kmpala baada ya wiki moja. Walipokuwa njiani, Masombo akapendekeza kwamba mkewe ajiunge na Chuo Kikuu cha Makerere ili kuendelea na masomo. Walipofika Kampala, mkewe akajaza fomu na kujiunga na Chuo Kikuu cha Makerere.

Nabuduwa akapambana na masomo. Kila wakati alikuwa maktabani. Masombo alijishughulisha na kazi ya nyumbani ili kumpa mkewe nafasi ya kusoma. Nabuduwa akamaliza kozi yake baada ya miaka mitatu na kwa sababu ya bidii yake pale chuoni na uhusiano mzuri na wahadhiri, akaajiriwa kuwa mhadhiri msaidizi pale chuoni.

## Sura ya 12

Baada ya miaka 6, wakanunua kijishamba pale jijini na kujenga jumba kubwa. Kabla kuhamia pale, wakaandaa karamu na kuwaalika wazazi wa mkewe. Nabuduwa akasafiri na Pajero lao na kuwaleta wazazi wake. Walikaribishwa kwa furaha na kuandaliwa vyakula pamoja na vinywaji tele katika karamu hiyo.

Mama mkwe akamwomba msamaha Masombo kwa ukatili waliomfanyia. Baba mkwe akalewa na kukatika. Baada ya wiki moja wakaamua kurudi kijijini. Masombo akawapa gari lao moja aina ya Premio ili watumie. Hiyo ilikuwa ni zawadi.

Mtoto wao alipofikia umri wa kupaswa tohara Masombo akaona aandae sherehe za tohara. Hata hivyo mkewe alitaka mtoto huyo atahiriwe hospitalini. Wakasafiri kwa Pajero yao hadi kijijnikuandaa sherehe hiyo ya tohara. Hata hivyo, Masombo alip[ogundua kwamba majirani walikuwa wamepanga kumroga kijana wake, akamwiita ngariba asubuhi moja kisirisiri na kumtahirisha bila wao kujua. Baada ya mwezi mmoja, wakarudi Kampala.

Urogi na uchawi katika jamii ya Masombo, ni jambo lililomsumbua. Aliona sasa ni jukumu lake, kuingilia kati na kubadili fikra za wanakijiji. Kwa sababu alikuwa na pesa, akaanza kuzitembelea shule za kwao na kufadhili wanafunzi werevu ambao walikuwa maskini. Wanafunzi hawa maskini, walilipiwa karo, kununuliwa vyakula na sare za shule. Vijana wengi kutoka sehemu hii yao walipata nafasi ya kusoma hadi vyuoni na kufanya kozi kadhaa. Sura ya Bukigai ikabadilka. Vijana hawa waliporudi kijijni walipiga vita fikra na Imani mbovu ya urogi, wivu, chuki n.k kupitia muziki na michezo ya kuigiza.

Masombo akaungana na mashirika yasiyokuwa ya kiserikali akapata misaada na kuinua elimu katika eneo mla Bukigai. Baadaye wazee wakaona mchanngo wa Masombo na kubadilisha fikra kumhusu. Siku nmoja wazee kwa vijana wakasafiri hadi kwake Kampala ili kuomba msamaha. Wazee hao waliandaa sherehe kabambe ya kujitakasa madhambi yao. Ngombe kadhaa walichinjwa na kutolewa kama kafara. Masombo na wazee wakanawa damu ya ngombe na kusameheana. Wakala, kunywa pombe pamoja na kucheza. Masombo akarudi Kampala baada ya siku mbili.

## Sura ya 13

Nabwire (bintiye Masombo) alimaliza chuo Kikuu na kufanya kozi ya ukatibu. Alitafuta kazi miaka kadhaa akashindwa. Waajiri walitaka kitu kidogo. Nabwire alisafiri hadi nchi jirani na kwa bahati akaajiriwa. Kwa sababu ya bidii yake, akapendwa sana na waajiri wake. Nabwire alikuwa ameolewa na kuzaa watoto wawili. Alimwandikia Masombo barua ilia je na mmewe, kumtembelea na kutambulisha mmewe kwao.

Ilibidi Masombo kusafiri hadi kijijini Bukigai ili kufahamisha watu wa ukoo wake wajitayarishe kuwapokea wageni. Wazee wakampongeza Masombo kwa kufanya sherehe zake kwa kuzingatia mila. Wazee wakaunda kamati andalizi, kisha Masombo akarudi Kamapala. Hata hivyo, kuanzia mwanzo, mkewe Masombo hakuunga mkono sherehe hiyo kupelekwa kijijini. Misimamo hii tofauti ilizua ugomvi na chuki kati ya Masombo na mkewe. Nabuduwa alipoona

Masombo pia amekasirika na hashughuliki naye, akalia na kuwa kama mwendawazimu. Wakasameheana na baada ya siku chache, Masombo akarudi kijijini kuwapelekea pesa za maandalizi.

### Sura ya 14

Masombo kwa mara ya kwanza akaona watu wa ukoo wake na majirani wakifanya kazi kwa furaha tena kwa ushirikiano pale kwake. Kwa hiari wakaamua kila mmoja kuchangia, ndizi, kuku, mbuzi na vyakula vya kila aina kufanikisha sherehe hiyo. Masombo akawanunulia mapipa ya pombe wakanywa huku wakiendelea na maandalizi. Baada ya siku nne Masombo akarudi Kampala ili kumleta mkewe.

Walipofika mjini Mbale wakanunua kreti 1000 za bia na 1000 nyingine za soda. Akakodi wanamziki kutoka mbale ili kutumbuiza wageni. Siku iliyofuata Nabwire akaingia na msafara wa Magari hamsini. Watu wa koo zote mbili wakajitambulisha. Wageni wakatoa zawadi kadhaa wakiwemo ngombe mia tano. Sherehe ikapamba moto kwa mlo vinywaji na dansi. Baadaye Masombo na mkewe wakarudi Kampala. Namuduwa akashangaa sana kuona jinsi majirani walikuwa wamebadilka.

Masombo na mkewe walipambana na kazi kwa bidii, na baada ya miaka 5 wakajenga ghorofa katikati mwa jiji, likaitwa Masombo na familia. Kijana wake wa kwanza akayasimamia majengo hayo. Baada ya kufanya kazi kwa miaka mitano Zaidi, wakastaafu. Wazee kwa vijana kutoka Bukigai wakamtembelea Masombo na kumshauri Masombo kugombea kiti cha ubunge katika eneo lao. Ingawa mkewe alipinga, majirani wakamhimiza asimame. Masombo akasimama kama mbunge na kupita bila kupingwa. Mkewe akafurahi. Kila mbunge alipewa jumba kubwa pamoja na gari.

Kwa bahati nzuri baraza la mawaziri lilipoundwa na Rais, Masombo akapewa uwaziri wa serikali za mitaa. Akajenga eneo bunge lake na kununua magari 20 ya kusafirisha watu katika eneo bunge lake bure. Masombo akasambaza umeme kijijini na hata mitambo ya kunasia stesheni za Radio, runinga na simu za rununu ikajengwa. Maji yalichimbwa, barabara kukarabatiwa na madaraja kutengenezwa. Maskini walijengewa nyumba za mabati. Watu wakampenda sana mbunge wao na kumpigia kura mfululizo. Akapewa kilima kimoja katika eneo lake na kujenga jumba kubwa. Akaamua kustaafu ingawa walitaka aendelee.

## MAUDHUI

1. **BIDII**

   - Masombo alionyesha bidii yake kila mahali; nyumbani, shuleni, kanisani, kazini,

bungeni n.k

- Masombo alifanya vibarua usiku na mchana kukimu familia yake.
- Alijiwekea pesa na kuamua kurudi shuleni.
- Bidii yake ilimfanya kupita mitihani ya kidato cha nne na cha sita.
- Mamake alipoondoka na kuwaacha wakiwa wachanga walifanya kazi pale nyumbani kwa bidii na kujitegemea.
- Hata walipolazimishwa kufunga ndoa, Masombo na Nabuduwa walifanya vibarua kwa majirani usiku na mchana ili kulea kitoto chao.
- Masombo alijenga nyumba ya mabati kutokana na bidii yake.
- Mamake Masombo alipoenda Mombasa, alifanya bidii na kujitajirisha. Alijenga jumba kubwa na kununua hata gari.
- Kwa sababu ya kusoma kwa bidii darasani, rafiki zake wakambandika jina Bwana mabuku.
- Masombo alipandishwa cheo kama Mwalimu Mkuu kutokana na bidii yake.
- Hata wazungu walimchagua kama katibu wa kamati tendaji katika shule ya chekechea kule Bukigai.
- Bidii yake masomoni ilimwezesha kusomea uzamili katika lugha ya Kiswahili na hata kuajiriwa kama mhadhiri katika chuo kikuu.
- Nabuduwa aidha aliporudi shuleni alipambana na masomo hadi akamaliza shahada. Kwa sababu ya bidii yake akaajiriwa kama mhadhiri msaidizi.
- Nabwire alipopata kazi, aliifanya kwa bidii na kupendwa sana na wakubwa wake. Alitajirika na kupata mme mzuri.
- Masombo alinunua viwanja jijini Kampala na kujenga maghorofa kwa sababu ya bidii yake.

## 2. ELIMU

- Mwandishi amedhihirisha kuwa elimu kweli ndio ufunguo wa maisha.
- Masombo alianzia shule ya msingi ya Bukigai, akaingia shule ya upili ya Masaaba, Nalwanza na Bukalasi.
- Aliendelea na masomo hadi chuo kikuu cha Makerere na baadaye Hussein Musa. Elimu ilibadilisha maisha yake.
- Chuoni Hussein Musa kulikuwa na Maprofesa wengi pamoja na madaktari, wahadhiri na wanafunzi waliofuzu katika taaluma mbali mbali.

- Masombo aidha alimuhimiza mkewe Nabuduwa kusoma hadi Makerere.
- Tunaona Masombo akiwafadhili vijana katika eneo lao Bukigai kimasomo.
- Kadhalika bintiye Masombo, Nabwire alisoma hadi Chuo kikuu na kupata kazi.
- Mwandishi pia ametutajia walimu wakuu wa shule mbali mbali, taasisi za elimu na vyuo ambapo elimu ilipewa kipaumbele.
- Mbali na kueneza neno la bwana, wazungu pia walifadhili miradi ya elimu.
- Inasemekana kuwa Mzee Kibeti pia alikuwa amesoma.
- Mwandishi ametuonyesha wazi kuwa elimu haina umri na wafanyao bidii masomoni ndio hufaulu.

### 3. UMASKINI

- Matatizo aliyopitia Masombo maishani yalitokana na hali kwamba alizaliwa katika familia maskini.
- Wazazi wake waliishi mashambani katika banda bovu ambalo lilifanya wachekwe sana.
- Ndugu yake mmoja alifariki dunia kwa kukosa pesa za matibabu.
- Namutosi, mamake Masombo aliuza pombe haramu, changaa ilia pate karo.
- Masombo aliripoti shuleni miguu mitupu. Tunaona hata akitembea kwa miguu hadi shuleni.
- Pale shuleni maisha yalikuwa magumu, alilala njaa kwa kukosa pesa.
- Shule ilipofungwa kwa ghafla, alitembea miguu hadi nyumbani.
- Masombo alipokamatwa mamake aliuza kila kitu akabaki uchi.
- Masombo na mkewe waliteseka sana. Hawakuwa na chakula, mavazi, dawa nk.
- Mkewe aliposhikwa na maumivu ya uzazi, walitembea kilomita kadhaa kutafuta huduma za hospitalini.
- Hata mtoto alipozaliwa, Masombo hakuwa na taulo, aliamua kutumia shati lake kuku.
- Kulea mtoto huyu kulikuwa shida, maziwa hayakuwepo na alipokuwa mgonjwa walitafuta mitishamba.
- Eneo zima la Bukigai lilikuwa na watu maskini, barabara zilikuwa mbovu, hakukuwa na nguvu za umeme na vile vile wanafunzi wengi hawakuendelea na masomo kwa sababu ya umaskini.

## 4. CHUKI NA WIVU

- Watu wa ukoo wa Masombo pamoja na majirani walichukia sana familia ya Mzee Kibeti. Chuki hii ilitokana na wivu waliokuwa nao.
- Masombo na msafara wa wageni wake walipoondoka kwenda kuhudhuria sherehe za kufuzu, majirani hawakufurahia.
- Mamake wa kambo pia alikuwa akimchukia Masombo na ndugu zake, aliwapiga na kuwanyima chakula.
- Pia kule shuleni wanafunzi walimchukia Masombo na kumwonea wivu. Siku moja Kutosi na wenzake walipanga njama na kumwaibisha darasani.
- Aidha masombo hakuwapenda wanafunzi hawa, na walimfanya hata kuchukia hisabati.
- Masombo alipoendelea na masomo yake watu wa ukoo wake waliona wivu. Ami zake hawataki kushirikiana naye kufanya kazi.
- Ami hawa walimchukia hata babake ati kwa sababu alikuwa na ngombe watano na kijishamba.
- Masombo alipopita mtihani na kujiunga na kidato cha kwanza, binamu zake walimchukia na kumwonea wivu. Walimnyima hata viatu.
- Walimu wa Masaaba vile vile walimchukia Mwalimu Mkuu. Walishirikiana na wanafunzi ili kuzua mgomo.
- Masombo alipopata kazi ya kufundisha majirani hawakufurahia.
- Walimwondoa Masombo katika kamati ya kusimamaia mradi wa kufuga ngombe wakidhani angekuwa tajiri kuwashinda.
- Aidha Masombo alimchukia sana Mwalimu Mkuu Mjanja.
- Tunawaona makasisi wengine wa kimwonea wivu Kasisi Mukhwana aliyependwa sana.
- Kasisi kibogoyo alipoletwa ili kuchukua nafasi ya Kasisi Mukhwana vile vile alichukiwa.
- Masombo alipoanza kuongoza ibada, makasisi wengine wakamchukia na kudai kuwa anapotosha wakristo.
- Walikataa hata kumuuzia Masombo shamba la kujenga kanisa, kwa sababu ya wivu.
- Wakristo na hasa viongozi hawakutaka Masombo ashiriki katika kamati yoyote.
- Hata walimu wenzake walikasirika Masombo alipofuzu na shahada ya uzamili.
- Majirani walianza kumfanyia Masombo urogi kwa sababu ya wivu.

## 5. WEMA

- Wahusika wengi katika riwaya hii wameonyesha ukarimu na wema wao.
- Joshua Kimanayi ambaye alikuwa Mwalimu Mkuu wa shule ya msingi ya Bukigai alimwokoa Masombo kwa kumpa kazi, na mshahara mara moja.
- Rafiki wa Masombo Omari Mzanzibari ndiye alimpa Masombo Benzi siku ya sherehe za kufuzu.
- Professa Bakari aidha aliwafadhili wanafunzi wengi kimasomo, pale chuoni Hussein Musa.
- Nabuduwa alipokuwa akiumwa na maumivu ya uzazi, alizalishwa na wanawake fulani wahisani pale hospitalini. Yule muuguzi alikuwa anataka hongo.
- Masombo aliporudi shuleni Nalwanza kuendelea na masomo, shule hiyo ilimfadhili na kugharamia kila kitu.
- Masombo alipopandishwa cheo kuwa Mwalimu Mkuu, alimwajiri alimwajiri adui wake wa zamani Mwalimu Mjanja. Alimpa hata laki tano za bure.
- Wazungu kutoka uingereza walifadhili makanisa na shule mbali mbali kwa ukarimu. Waliwatumia wakristo pesa za misaada.
- Masombo aidha hakuharibu pesa za misaada, alihakikisha kuwa amewasaidia watu wa eneo lake.
- Daktari Musinguzi na Kiplimo James walimlipia Masombo karo aliposhindwa na kumletea vitabu kutoka maktaba ya vyuo mbali mbali.
- Karimu na Bi Fatuma pia walimsaidia sana Masombo na mkewe. Walimpa gari bure na kumhamisha mkewe kutoka Nakapiripirit hadi shule ya msingi ya Naguru.
- Masombo aidha aliwapa wazazi wa mkewe gari na kuwasamehe.
- Masombo alipopata pesa nyingi aliwalipia karo vijana wengi kutoka kwao.
- Katika sherehe ya Nabwire kumkaribisha mmewe wanakijiji pia walichangia mikungu ya ndizi na ndizi.
- Wageni wa Nabwire aidha walitoa zawadi nyingi wakiwemo ngombe mia tano kwa wazee.
- Masombo alipochaguliwa kuwa mbunge, alileta maendeleo mengi na kuwa kielelezo cha uongozi bora.
- Nduguye Masombo, Mwema aidha alikuwa mkarimu na alimsaidia sana Masombo na mkewe.
- Kwa jumla fanaka za Masombo zilitokana na ukarimu wake.

## 6. NDOA NA MAPENZI

- Kumechorwa ndoa nyingi humu riwayani.
- Mzee kibeti alikuwa na wanawake wawili, Namutosi ambaye alikuwa mamake Masombo na Mama wa kambo.
- Aidha Masombo alikuwa na wapenzi wengi akiwa kijana barubaru. Alimwoa Nabuduwa wakiwa kidato cha tatu.
- Masombo aidha alipendwa na mamake pamoja na mwalimu wake wa Hisabati pale shuleni.
- Masombo alipokuwa kijana barubaru, aliwapenda wasichana wengi akiwemo Sijali.
- Wanafunzi wengi wa shule ya wavulana ya Masaaba walifanya mapenzi na wasichana wa shule ya upili ya Budadiri.
- Masombo alipopata pesa alinunulia mkewe, mtoto na mamake nguo – kudhihirisha mapenzi yake.
- Wazungu na wafadhili kutoka ngambo walimpenda sana Masombo.
- Masombo vile vile alimpenda sana Nabuduwa baada ya ndoa, aliwachana kabisa na wasichana wengine.
- Masombo na mkewe walimpenda sana Namutosi (mama yao). Walisafiri hadi Mombasa kumtembelea.
- Mamake Masombo aliuza kila kitu ili kumwokoa mtoto wake aliposhikwa.
- Nabwire kadhalika alikuwa kaolewa na kuzaa watoto wawili.
- Baadaye wenyeji wa Bukigai walibadilika na kumpenda sana Masombo na hata kumchagua kuwa kiongozi wao. Walimpa hata kilima kimoja akajenga nyumba.

## 7. UTAMADUNI, MILA NA DESTURI

- Sherehe nyingi zilifanywa kwa kuzingatia mila za mhusika mkuu, kwani mwacha mila ni mtumwa.
- Mzee shibita aliitwa aliitwa ili ampe jina bintiye Masombo. Alimchinja mbuzi beberu na kufanya kafara ili kuwasiliana na mababu kabla jina kutolewa.
- Kijana fulani aliyemuuzia Masombo shamba aidha alikuwa amevunja mwiko. Alioa mke na kuishi naye kwa wajomba jambo ambalo lilikuwa kinyume na desturi zao. Watoto wake walianza kufa mmoja baada ya mwingine.
- Mtoto wa Masombo mvulana pia alitahiriwa kimila kwa kisu cha ngariba na kupewa

maelekezo.

- Wavulana waliotahiriwa hospitalini kutoka jamii hiyo walidharauliwa na kuchukuliwa kuwa wanawake.
- Wazee walipogundua kwamba walimchukia bure Masombo, waliandaa sherehe kabambe kimila ili kujitakaza dhambi zao. Ngombe walichinjwa wakanawa damu.
- Kadhalika Masombo aliandaa sherehe ya kumtambulisha mmewe Nabwire kwa wazee kwa kuzingatia mila na utamaduni wao.
- Wanaume walivaa kanzu na koti ilihali wanawake walivaa gomasi.
- Kitamaduni waliamini kwamba mtoto ni wa ukoo na jamii nzima.
- Kufuatana na utamaduni wa akina Masombo, mwanamke hakuruhusiwa kuzungumza mbele ya kikao cha watu.
- Wanakijiji walikunywa gongo na kucheza nyimbo za kijadi.
- Wakwe hawakuruhusiwa kukaa ukweni hadi usiku.k.m Mmewe Nabwire.

## 8. DINI, IMANI NA ITIKADI

- Jamii ya Masombo ilikuwa na Imani katika mababu, miungu na hata dini za Kimagharibi.
- Mzee kibeti na mkewe Namutosi walikuwa wakristo katika kanisa la kiangilikana kule Bukigai.
- Bila shaka Masombo naye alijiunga na kanisa hilo akawa mshiriki wa dhati.
- Neno la bwana lilitangulizwa kabla sherehe au shughuli yoyote. Tunamwona Masombo akiomba kabla msafara wake kufuatana hadi chuoni kwa sherehe.
- Kule chuoni, mahema yalipangwa kijinsia kwa sababu katika chuo hicho cha Kiislamu wanafunzi hawakuruhusiwa kutangamana wasichana kwa wavulana.
- Hata kabla ya sherehe ya kufuzu kuanza, maombi yalitangulia.
- Namutosi aliomba mababu haswa Masaaba awaongoze Masombo na mkewe hadi hospitalini bila hatari yoyote.
- Masombo alipokuwa Mwalimu Mkuu, aliongoza ibada na kushirirki kazi nyingi za kanisa.
- Masombo alifungua tawi la kanisa hilo mbale ili kueneza injili.
- Inasemekana mkewe Nabuduwa alikuwa mwokovu, na aliombea familia yao kila siku.
- Masombo aliwahi kujiunga tena na dhehebu la Wakristodeliphiano.

- Wazee wa Bukigai waliamini kuwa Masaaba ndiye alikuwa mwanzilishi wa jamii hiyo.
- Wazungu walifadhili dini mbalimbali na kujenga makanisa.

## 9. USHAMBA

- Raia wa Bukigai walikuwa hawajastaarabika, waliamini sana mambo ya urogi na uchawi.
- Masombo alipowaletea kreti za bia walikuwa hawajawahi kuziona.
- Pia walishangaa kuona magari makubwa makubwa na kila mara walitamani kupewa lifti.
- Hata mitambo ya muziki ilipofika pale Bukigai walishangaa sana.
- Walidhania kuwa chupa za bia (Nile) zilikuwa ni za madawa. Walipoionja pombe hii walitapika.
- Ushamba huu uliwafanya kuoneana wivu, kuchukiana na kubaki nyuma kimaendeleo. Hata wanakijiji wengine wakaanza uchawi na urogi.

## 10. UROGI NA UCHAWI

- Raia wa Bukigai waliamini sana katika urogi.
- Mtoto wa Mzee Kibeti alipougua homa ya malaria na kufa, aliamini kwamba amerogwa.
- Baada ya Masombo kumaliza shahada yake ya uzamili, majirani waliona wivu sana. Walianza kuzika mitishamba katika boma lake ili kuidhuru familia yake.
- Aidha kijana wake alipotaka kutahiriwa, majirani walipeleleza ili wamroge.
- Hata Masombo mwenyewe anadai kuwa urogi na uchawi ni jambo lililomsumbua akaamua kuingilia kati.

## 11. FITINA

- Masombo alipolazimishwa kuoa akiwa na umri wa miaka 15 majirani walimfitini Nabuduwa ili kumwacha bwanake maskini.
- Kasisi Mukhwana vile vile alifanyiwa fitina na kuhamishwa kutokana na wivu wa makasisi wengine.
- Masombo alipotaka kuanzisha tawi la kanisa mjini Mbale, Nabende alimfanyia fitina kwa mzungu akidai kuwa Masombo ni mbinafsi na si kiongozi mzuri.

- Pia anadanganya kwamba Masombo humpiga mkewe kila siku.
- Binamu yake Masombo pia aliporuhusiwa kushiriki nao katika kanisa la Mbale, alianza kumwendea Masombo kichinichini hadi akafukuzwa.

**12. UONGOZI MBAYA**

- Baadhi ya viongozi katika riwaya hii wamechorwa kuwa wenye ubinafsi, ufisadi, wivu na wanaotaka kujitajirisha haraka.
- Kutokana na uongozi huu mbaya, eneo la Bukigai lilbaki nyuma kimaendeleo; hakukuwa na umeme, barabara nzuri n.k eneo bunge hili lilibadilika tu baada ya Masombo kuingia bungeni.
- Mwalimu Mkuu Mjanja alikuwa mjanja kama jina lake mwenyewe. Alipanga njama na kuwaibia walimu pesa.
- Kamati ya kusimamia misaada kanisani pia, iliwaibia wakristo pesa zao kutoka ngambo. Viongozi hawa walitoa ripoti na risiti bandia za matumizi ya pesa.
- Kusolo aliyekuwa mwenyekiti alishirikiana na wenzake wakala hata pesa za kuwakaribisha wazungu.
- Aidha Masombo alipoingia uongozini, alishirikiana na wanakamati wengine wakatumia pesa za kanisa kwa shughuli binafsi.

**13. UFISADI**

- Afisa wa polisi anapokea laki saba ili kuifililisha kesi ya Masombo ya kumtunga msichana mdogo mimba na kumshambulia polisi.
- Wazazi wa Nabutuwa kadhalika walipokea kitu kidogo na kutupilia mbali kesi hiyo.
- Askari wa lango pale hospitalini pia alipewa na Masombo shilingi elfu ndipo akawaelekeza kwenye wadi.
- Mkunga vile vile anataka hongo, kabla kumhudumia Nabuduwa.
- Nabwire alipomaliza kusoma alitafuta kazi kwa miaka kadhaa lakini hakufaulu,waajiri walikuwa wanataka hongo.

**14. USHIRIKIANO**

- Waswahili husema umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu.
- Riwaya inapoanza tunaona Masombo akishirikiana na jamaa na marafiki wakifanya kazi ya kuandaa sherehe yake ya kufuzu pamoja na karamu.

- Pale shuleni, Masombo na wenzake walisaidiana kimasomo hadi darasa la saba na wakapita mtihani wote.
- Masombo alishirikiana pia na majirani kufanya kazi ingawa walimchukia.
- Kanisani alishirikiana na wakristo pamoja na wanakamati kueneza injili.
- Alipotaka kufungua tawi la kanisa hilo mjini Mbale, alishauriana kwanza na Mathias.
- Katika sherehe mbali mbali pale kwa Masombo, wanakijiji walishirikiana naye na hata kuchangia vyakula.
- Umoja huu ndio ulimfanya Masombo kuingia bungeni bila kupingwa.

## 15. DHULUMA

- Baadhi ya wahusika walikuwa wadhalimu na waliwatendea wenzao maovu.
- Mzee Kibeti na mkewe Namutosi walivurugana hadi Namutosi akatoroka kabisa wakiwa wadogo.
- Mama wa Kambo aliwafanyisha kazi ngumu kama punda, akawatusi pamoja na kuwapiga.
- Masombo na ndugu zake walinyimwa chakula na hata kulala njaa.
- Mwalimu Mjanja alitumia ujanja wake kuwaibia walimu mishahara yao.
- Hata jina la Masombo liliondolewa katika daftari la malipo, na pesa zake kuchukuliwa.
- Masombo alipofuatilia mshahara wake, akapoteza kazi kabisa.

## 16. UTAJIRI

- Baadhi ya wahusika walikuwa matajiri kupindukia.
- Masombo aliporipoti kidato cha kwanza, aliona wenzake wakifika shuleni katika magari ya kifahari.
- Wanafunzi hawa kutoka familia tajiri hawakuridhika na vyakula pale shuleni.
- Pia Nabuduwa akiwa shuleni alikuwa akitoroka na Masombo na kumfadhili mjini Mbale katika raha zao na burudani.
- Kadhalika baadaye, Masombo alitajirika na kumiliki majumba makubwa, magari na viwanja kadhaa jijini Kampala. Aliishi kama mzungu.
- Mamake Masombo na bintiye aidha walitajirika kutokana na bidii zao maishani.
- Inasemekana wabunge walipewa magari na majumba makubwa.

## 17. MABADILIKO

- Baada ya shule ya upili ya Masaaba kufungwa kwa ghafla, Mwalimu Mkuu aliboresha vyakula, burudani shuleni na michezo mipya kuanzishwa.
- Masombo alipofika kidato cha 3, alibadilika kitabia na kuanza kufuatilia wasichana.
- Masombo pia alibadilika na kuwa mdanganyifu. Hakumweleza mamake ukweli.
- Hata hivyo, alipooa alibadilika na kuachana na wasichana kabisa.
- Masombo alikuwa mwokovu, lakini wakati mwingine alishirikiana na wanakamati wahalifu na kuwaibia wakristo pesa za kanisa.
- Mwalimu Mkuu mjanja pia pesa zilimwisha akawa maskini mfyeka nyasi.
- Masombo alibadilika na kuhamia katika kanisa la Wakristadeliphiano.
- Wanakamati wa kusimamia kanisa walibadilishwa kila wakati.
- Wakristo na wanakijiji kwa jumla walikuwa ni watu wasiokuwa na msimamo katika jambo lolote. Walikuwa wakibadilikabadilika.
- Maisha ya Masombo na mkewe yalibadilka. Umaskini waliokuwa nao uliisha wakaishi kama matajiri.
- Mamake Masombo pia alipata nafuu akafanikiwa maishani.
- Wanakijiji walibadilika wakawa wazuri.
- Wazazi wa Nabuduwa walibadilika wakawa wazuri.
- Mbunge wa Bukigai, mheshimiwa Masombo alibadilisha eneo zima la Bukigai kimaendeleo.

## 18. UKOSEFU WA NIDHAMU

- Masombo aliingilia mapenzi akiwa mdogo, wanakijiji wakalalamika sana. Alikuwa akijifungia vyumbani na wasichana hata wakati wa mchana.
- Shule ya upili ya Masaaba na ile ya wasichana ya Budadiri ilikosa maadili mema. Wasichana na wavulana wa shule hizi walifanya mapenzi kiholela.
- Masombo na Nabuduwa walikuwa wakihepa shuleni usiku usiku kwenda mjini kula raha.
- Masombo alishambulia Mwalimu Mkuu na hata Polisi kwa kukosa maadili.

## 19. STAREHE

- Masombo aliandaa karamu kubwa baada ya kufuzu. Walikuia wakanywa na kuburudika kwa starehe.
- Mzee Kibeti na majirani wenzake walipenda kunywa gongo na kustarehe.
- Masombo alipokuwa akihamia kwa nyumba yake mpya, alitayarisha karamu kem kem na kuwaalika wakwe zake, wakanywa na kuburudika.
- Aidha Nabwire alipomleta mmewe kwao, Masombo aliandaa sherehe ya kupigiwa mfano. Watu walikunywa mapipa ya gongo wiki zima, pamoja na kreti za bia na soda.
- Vile vile Masombo aliwaandalia wanakijiji sherehe kubwa pale jijini Kampala.

## WAHUSIKA:

### 1. MASOMBO

Ni mwanawe Mzee Kibeti na Bi Namutosi. Pia ni mmewe Nabuduwa na kakake Mwema.

(a) **Msomi**; alisoma hadi chuo kikuu na kusomea kozi wa uzamili katika lugha ya Kiswahili.

(b) **Mwenye Bidii**; Alifanya  kazi kwa bidii pale nyumbani, kazini na hata kanisani.

(c) **Maskini**; alitoka katika familia maskini, akateseka sana.

(d) Mvumilivu; Alipata shida nyingi pale nyumbani, shuleni, kazini na hata kanisani lakini akavumilia.

(e) **Mwokovu**; kuanzia utotoni alishiriki katika kanisa la kiangilikana. Aliongoza hata ibada.

(f) Mwenye mapenzi ya dhati; aliachana na wasichana wengine na kumpenda mkewe Nabuduw kwa dhati.

(g) **Mkarimu**; aliwasaidia jamaa na marafiki alipopatanafasi. Aliwasaidia sana jirani zake.

(h) Mwerevu; alikuwa mwerevu sana darasani hadi akachukiwa na kuonewa na wenzake darasani.

(i) **Mwenye hasira**; alipandwa na hasira na kuzua vita kila wakati, k.m shuleni anampiga Mwalimu Mkuu na hata Polisi.

(j) **Mwenye Ushirikiano**; alishirikiana na wenzake pale nyumbani, shuleni, kanisani na hata kazini.

(k) **Mtamaduni**; alifanya sherehe kulingana na utamaduni wao. K.m kuwapa watoto majina, tohara, na sherehe za kutambulisha wakwe.

(l) **Mnadhifu**; alipenda sana usafi, hivyo alipendwa sana na wasichana.

(m) **Mtetezi wa haki**; alitetea haki zake na za wenzake. Hata bungeni alitendea raia wa Bukigai haki.

(n) **Kiongozi bora**; alikuwa kielelezo cha viongozi bora bungeni.

(o) **Mkweli**; alipopewa wadhifa, aliwajibika na kutenda kazi yake kwa haki na ukweli.

(p) **Mfadhili**; alipotajirika aliwasaidia vijana kutoka eneo lake kwa kuwalipia karo.

2. <u>MZEE KIBETI</u>

Ni mmewe Namutosi na babake Masombo.

(a) **Maskini**; alikuwa mzee maskini, na hivyo watoto wake waliteseka sana.

(b) **Mlevi**; alipenda ulevi wa gongo na starehe.

(c) **Mzembe**; uzembe wake ulipelekea mtoto wake mmoja kufa homa ya malaria.

(d) **Mshirikina**; aliamini katika uchawi, ndiyo maana hakumpeleka mtoto wake hospitalini.

(e) **Msomi;** alisoma hadi darasa la tano.

3. <u>NAMUTOSI</u>

Ni mkewe Mzee Kibeti na mamake Masombo na wengine.

(a) **Maskini**; alikimu familia yake kwa kuuza changaa. Pia aliuza kila kitu na kutembea uchi ili amwondoe Masombo kizuizini.

(b) **Mwenye mapenzi**; aliwapenda watoto wake sana, alihakikisha kuwa wanakula na kwenda shuleni.

(c) **Aliyewajibika**; alitimiza mahitaji ya watoto wake licha ya umaskini.

(d) **Mwenye bidii**; aliuza pombe haramu na kufanya vibarua ili kutunza watoto wake. Bidii yake mjini Mombasa ilimfanya kutajirika.

(e) **Mvumilivu**; alivumilia shida alizopitia na familia yake pamoja na majirani waliowachukia.

(f) **Mshauri**; alimshauri Masombo kwa hekima na kumhimiza afanye bidii maishani.

(g) **Mwenye huruma**; alimhurumia Masombo aliposhikwa. Aliuza kila kitu.

(h) **Mwokovu**; alikuwa mshiriki katika kanisa la kiangilikana

4. <u>NABUDUWA</u>

Ni mkewe Masombo.

(a) **Msomi**; Liicha ya kupata mimba, alirudi shuleni na kuendelea na masomo.

(b) **Kiongozi**; alikuwa kiranja mkuu wa wanafunzi kule shuleni.

(c) **Tajiri**; alitoka katika familia tajiri. Baadaye pia alitajirika kivyake na mmewe.

(d) **Mwenye bidii;** alifanya vibarua na mmewe ili kujikimu kimaisha.

(e) **Mwenye chuki;** kila wakati alichukiwa mmewe kwa kutomuunga mkono katika maswala mbalimbali.

(f) **Mwokovu**; alikuwa mcha Mungu na aliomba kila wakati.

5. <u>NABWIRE</u>

Mwanawe Masombo na Nabuduwa

(a) **Msomi;** alisoma hadi chuo kikuu.

(b) **Mwenye bidii**; alikuwa na bidii masomoni na hata kazini.

(c) **Mtamaduni** ; alizingatia mila za kwao.

6. <u>MWEMA</u>

Ni nduguye Masombo, mwanaye Kibeti na Namutosi.

(a) **Mwema**; alimsaidia Masombo akiwa kizuizini na pia wakati mkewe aliumwa na maumivu ya uzazi.

7. <u>KARIMU</u>

Alikuwa jirani yake Masombo.

(a) **Mkarimu**; alimkaribisha Masombo na mkewe kwa chakula. Aliwapa gari la kutumia na kusaidia kuhamisha mkewe hadi Naguru.

*MWISHO*